MAJARIBIO YA MTIHANI
DARASA LA 5 MUHULA WA MWISHO 2006
KISWAHILI

Soma kifungu kifuatacho kina nafasi 1 - 15. Tumia maneno uliyopewa hapo chini kujaza mapengo

Nchi ____1____ Kenya imegawanyika _____2_____ mikoa _____3____. Kuna mkoa ____4_____ pwani, mkoa wa mashariki, mkoa wa kaskazini mashariki ____5____ wa kati, mkoa wa bonde la ufa, mkoa wa magharibi _____6_____ wa Nyanza _____7____ mkoa wa Nairobi ____8____ wa ____9____ huitwa pisii, ____10____ mkoa umegawanywa _____11____ wilaya kadhaa. ____12____ wa wilaya huitwa ____13____ na kila _____14____ imegawanywa katika ____15_____ kadha.

1.	A. wa	B. kwa	C. kenywe	D. ya
2.	A. ndani	B. katika	C. kati	D. katikati
3.	A. minane	B. minne	C. manane	D. nane
4.	A. ya	B. kwa	C. kwenye	D. wa
5.	A. mkoa	B. mukowa	C. mukoa	D. mikoa
6.	A. mukoa	B. mikoa	C. mkoa	D. mukowa
7.	A. nao	B. na	C. nayo	D. nacho
8.	A. mguu	B. mkuu	C. mku	D. muku
9.	A. nchi	B. mukoa	C. mkoa	D. mukuwa
10.	A. na	B. ila	C. kila	D. nalo
11.	A. kwenye	B. kila	C. kwa	D. kati
12.	A. mku	B. pisii	C. mguu	D. mkuu
13.	A. dioo	B. mkuu	C. pisii	D. disii
14.	A. mkoa	B. wilaya	C. tarafa	D. pisii
15.	A. tarafa	B. taifa	C. mitaa	D. jiji

Chagua neno lifaalo

16. Kulala chali ni _____.
    A. kulala usingizi
    B. kulala uso ukielekea chini
    C. kulala uso ukiangalia juu
    D. kulala na kuota ndoto
17. Aliyesimama _____ mlango ni nani?
    A. kabla ya B. mbele ya
    C. juu ya D. baada ya

Kanusha sentensi zifuatazo

18. Ndege amepaa mtini.
    A. ndege hakupaa mtini
    B. ndege hajapaa mtini
    C. ndege hatapaa mtini
    D. ndege hawajapaa mitini
19. Mama alishona nguo.
    A. mama alirarua nguo
    B. mama hakushona nguo
    C. mama hajashona nguo
    D. mama hawajashona nguo
20. Akisami
    Robo ni sawa na _____
    A. $^1/_3$ B. $^1/_4$ C. $^1/_5$ D. $^1/_6$

Andika sentensi zifuatazo kwa wingi

21. Baba alisema atakuja
    A. mababa walisema watakuja
    B. baba alisema watakuja
    C. baba walisema watakuja
    D. baba walisema hawatakuja
22. Ukija kwake hutampata
    A. mkienda kwake hutampata
    B. mkija kwao hamtawapata
    C. ukija kwao hutampata
    D. ujika kwao hamtampta
23. Umbo hili laitwaje?

    A. mraba
    B. pia
    C. mstatili
    D. pembe tatu
24. Andika tarakimu ifuatayo kwa maneno.
    2,621
    A. elfu mbili, sitini na mbili na moja
    B. elfu ishirini, mia na ishirini na moja
    C. elfu mbili mia, sitini na mbili na moja
    D. elfu mbili, mia sita na ishirini na moja

Kamilishi methali ifuatayo

25. Haraka haraka haina
A. balaka B. hasara
C. baraka D. haraka

26. Upande ulioonyeshwa kwa mshale ni

A. mashariki
B. kusini
C. magharibi
D. kaskazini

Tegua vitendawili vifuatavyo

27. Ukoo wetu daima uko safarini
A. samaki B. siafu C. chura D. nyota

28. Apitapo huacha alama
A. konokono B. garimoshi
C. mzige D. kobe

29. Andika neno moja badala ya maneno uliyopewa machungwa, maembe, ndizi, paipai
A. miti B. mimea
C. matunda D. chakula

Tumia "pi" kwa usahihi 30 - 34

30. Mwalimu wataka kalamu _____?
A. ipi B. gani C. wapi D. yupi

31. Ni vikombe _____ vilivyovunjika?
A. zipi B. vipi C. gani D. ipi

32. Kitabu _____ kina hadithi tamu tamu?
A. gani B. kipi
C. yupi D. viganii

33. Ni darasa _____ lina watoto wengi?
A. ipi B. lipi C. wapi D. zipi

34. Ni mwanafunzi _____ aliyetunzwa?
A. gani B. ipi C. yupi D. wapi

35. Twasema giza _____
A. tororo B. totoro C. ndi D. zi

36. Maziwa yote yamemwagika.
A. mwa B. ndii C. pu D. zi

37. Mmea unaozaa nyanya waitwaje?
A. mtungule B. mnyanya
C. mmea D. karafuu

38. Mtu anayetengeneza pombe akitumia nazi huitwa
A. mnazi B. mgema
C. mpikaji D. nakoa

39. Ni saa ngapi?



A. saa kumi na mbili na dakika nne
B. saa nne kamili
C. saa kumi kamili
D. saa moja kasorobo

40. Utamwitaje mtu ambaye majina yenu yanafanana?
A. somo B. wifi
C. kaka D. mjomba

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo 41 - 50

Michezo ina faida kwetu sisi. Mbali na kuifanya miili yetu iwe na afya, michezo ina faida nyingi. Humsaidi mtu kuupitisha wakati wake vizuri badala ya kuyaingilia mambo yasiofaa.

Si lazima mti awe na kipawa maalum katika michezo. Mtu yeyote anaweza kushiriki katika michezo mbalimbali. Wakati mzuri wa kufanya michezo ni baada ya shule au baada ya kazi.

Michezo ina faida sana kwa wanafunzi. Humsaidia kuwa na nidhamu maishani. Huwafunza kuwa mtu hawezi kushinda kila wakati. Vile vile huwasaidia kushirikiana na wenzao kutoka sehemu mbalimbali za nchi, kwa njia hiyo umoja baina ya makabila mbalimbali huendelezwa. Ukabila huondoka.

Wanaotia bidii michezoni hupata nafasi za kusafiri kwenda nchi za ng'ambo. Hali kadhalika wanaoshinda hujipatia **tuzo** mbalimbali. Wengine hujipatia **vikombe** na kuiletea nchi yao sifa. Kwa hivyo michezo ina faida kubwa kwa wanafunzi watu wazima na nchi yote kwa jumla. Wasichana na wavulana wamejitahidi sana michezoni. Wakati ambao michezo ilikuwa ya wanaume pekee umeisha kupita.

41. Faida nyingine ya michezo ni kumwezesha mtu
A. kupata mali
B. kupumzika
C. kuwaogopa wenzake
D. kuupitisha wakati wake vizuri

42. Ni watu gani wanaoweza kushiriki katika michezo
A. watu wote B. wazee
C. wanaume D. wanawake

43. Wakati mzuri wa kufanya michezo ni
A. wakati wowote B. baada ya kazi
C. asubuhi D. mtu anapoamka

44. Michezo huwasaidia wanafunzi kuwa
A. wakatili B. wavivu
C. wajinga D. na adabu

45. Michezo huwafunza wanafunzi kuwa
A. lazima washinde
B. uvivu ni lazima
C. ushindi haupatikani kila siku
D. wazee hawafai kucheza

46. Umoja hupatikana
A. wanafunzi wa kabila moja wakikutana
B. wanafunzi wa makabila tofauti wakikutana
C. wazee wakishindana na vijana
D. wanafunzi wakishindana na wanaume

47. Wanaotia bidii michezoni
A. hupata nafasi za kusafiri nchi ngambo
B. hutatizika maishani
C. hujikwaa
D. hushindwa masomoni

48. Asiyekubali kushindwa
A. hushindwa B. simshindi
C. ni mshindi D. hashindwi

49. Neno **'tuzo'** lina maana gani?
A. adabu B. zawadi
C. mziwa D. bidii

50. Kichwa kinachofaa kwa habari hii ni?
A. michezo B. wanariadha
C. kandanda D. ushindi